SHULE YA UPILI, MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

# MTIHANI WA MWIGO, 2024

**102/2** **Kiswahili - Lugha** **Karatasi ya 2**

**Juni, 2024** **Saa 2½**

Jina: MWONGOZO .................................................. Nambari: ..................

Mkondo: ............................ Sahihi: ...................

**102/3 Kiswahili – Fasihi**
Jumatano Tarehe 3 Juni, 2024
Adhuhuri
Saa 2-4.30Adhuhuri

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Andika mkondo wa kidato chako kisha tia sahihi yako na uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali yote.*
*(d) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(e) Majibu yote **sharti** yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***(g) Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
***(h) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

## 1. UFAHAMU(ALAMA 15)

a) wenyeji kunyonga Kiswahili
Wageni kutambua utamu wa Kiswahili na kujifunza ilihali wenyeji wanakipuuza
(ii) Wageni kutumia Kiswahili kwa njia inayopendeza.
(iii) Wageni kujistawisha katika Kiswahili na wengine wakawa walimu. (3×1=3)
(b)(i) Kutia kiasi kichache cha habari katika magazeti ya Kiswahili.
(ii) Kuuza magazeti kwa bei ya chini mno.
(iii) Ukosefu wa utamu katika magazeti ya Kiswahili.
(iv) Mtazamo kuwa magazeti ya Kiswahili yanafaa kusomwa na wazee au walioshindwa na masomo shuleni.
(v) Vipindi vingi kwenye runinga kuwasilishwa kwa Kiingereza.
(vi) Watangazaji kwenye runinga kuhoji na kualika wahojiwa wasiokijua na kukmudu Kiswahili kuzngunza mada husika.
(3×1=3)
(c)(i) Kiswahili kufanywa lugha rasmi.
(ii) Wanasiasa kutumia Kiswahili bungeni akiwemo rais.
(iii) Sera zinazohusu elimu zikaranitiwe ili Kiswahili kitumiwe kwa upana.
(3×1=3)
(d)(i) Kiswahili kinafunzwa katika vyuo vikuu Marekani na Ulaya.
(ii) Kiswahili kimepitishwa kama lugha mojawapo ya zile rasmi katika vikao vya Jumuiya ya Afrika. (alama2×1=2)
(f) kiswahili kimepewa matumizi finyuu kama lugha rasmi huku kiingereza kikipewa matumizi mapana.
2/0
e) (i) nyeti –muhimu
Kukwepua miliki- kuiba mali ya wenyewe (2×1=2)

## 2. UFUPISHO (AlAMA 15)

a) -Bei ghali ya vyakula ni jambo linalowaathiri wakenya wengi.
-Familia nyingi nchini hukosa lishe.
-Kwa muda mrefu, viongozi wamekuwa wakipambana na tatizo la uhaba wa chakula
-Chakula kinachotumwa na serikali hakitoshi.
-Kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi ndicho chanzo cha uhaba wa chakula.
-Zipo sehemu nyingi nchini ambazo ni kame.
-Wengine wanapokosa chakula kabisa huazimia kula visivyoliwa.
-Mbinu hasi za kilimo husababisha utoaji wa mavuno haba.
-Wakulima wengine hukaidi wito wa kupanda mimea inayostahimili ukame.
-Baadhi ya wakazi hawana mwao kuhusu umuhimu wa lishe bora

b) -Kupunguza bei ya mbolea hadi sh. 3500.
-Uchimbaji wa visima na mabwawa ya maji
-Kupanda mimea inayopevuka na kutoa mazao haraka.
-Kuanzisha miradi ya ufugaji wa kuku wa kututumuliwa.
-Kutumia njia za kisasa za kuzalisha na kuhifadhi chakula.
-Wakulima wajiasi dhidi ya kuuza vyakula kwa bei ya chini.
-Wanaoishi sehemu za vinamasi wasaidiwe kutunza sehemu hizi.
-Vijana wahimizwe kuwaunga wazee mkono kushughulikia kilimo mashambani.

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**a)** Tenganisha silabi katika neno **wamnyweshayo.** (alama 1)

wa – m – nywe – sha – yo 1/0

**b)** Andika neno lenye mpangilio ufuatao wa sauti. (alama 1)

Sauti wastani viringe, sauti mwambatano ya kaakaa gumu, sauti ya chini ...Onywa... 1/0

oshwa

**c)** Geuza sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha bila kurudia kitenzi -fanya. (alama 2)

Neto alimfanya Salim kuzoa takataka nyingi.

Neto alimzolesha Salim takataka nyingi 2/0

**d)** Ainisha vitenzi katika sentensi: (alama 2)

Watu warefu kupindukia ndio waliokuwa hapo jana.

Ndio- Kitenzi kishirikishi kipungufu 1x1

waliokuwa - kitenzi kishirikishi kikamilifu 1x1

**e)** Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Huzuni alipongezwa kabla ya kufuzu mtihani

Huzuni alikashifiwa baada ya kufeli mtihani 1/0

alikezwa
alikemewa
alikejeliwa

**f)** Akifisha kifungu hiki. (alama 3)

tanzu maigizo hadithi ngano tanzu za fasihi simulizi zote huburudisha wakenya sana

Tanzu: Maigizo, hadithi/ ngano (tanzu za fasihi simulizi zote) huburudisha Wakenya sana. 6x½=3

**g)** Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya kivumishi cha pekee hali ya kusisitiza. (alama 2)

-enyewe

Mchuuzi mwenyewe amesafiliwa. 2/0

**h)** Andika katika wingi. (alama 2)

Mbuzi wa jirani yake aliibwa na mtu aliyekamatwa na polisi.

Mbuzi wa majirani zao waliibwa na watu waliokamatwa na polisi 2/0

wao

14

i) **Tumia kielezi kiigizi badala ya kile kilichopigiwa mstari.** (alama 1)

**Mbwa yule alibweka <u>kwa hasira.</u>**

Mbwa yule alibweka bwe! bwe! 1|0

j) **Tambua aina ya virai katika sentensi ifuatayo:-** (alama 2)

**Gharama ya maisha imekuwa ghali kupindukia.**

Gharama ya maisha – RN ghali kupindukia – RV

Ya maisha – RH RE – Kupindukia 4×½=2

Imekuwa ghali kupindukia – RT


k) **Bainisha majukumu ya mofimu zinazounda neno: yaliyochika:** (alama 3)

Ya — li — yo — ch — ik — a 6×½=3

Ngeli wakati urejeshi mzizi kauli kiishio.

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya **matawi.** (alama 4)

Wachache <u>waliokuwa wagonjwa</u> w<u>alitibiwa na daktari</u>.




m) **Andika katika usemi wa taarifa.** (alama 2)

**"Ala! Nani amekikirarua kitabu changu hivi?" Sabina akasaili.**

Sabina alishangaa na akataka kujua aliyekuwa amekikirarua kitabu chake vile. 4×½=2

n) **Bainisha matumizi ya kiambishi 'o' katika sentensi ifuatayo.** **(alama 2)**

**Luka aliimba wimbo uliowavutia wengi.**

Wimbo – unominishaji 1x1

uliowavutia – urejeshi. 1x1

o) **Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:** **(alama 2)**

**Nomino + RH + Kitenzi + Kipozi**

Halaiki ya watu ilimpiga mwizi 2/0

p) **Tambua uamilifu wa neno vile katika sentensi ifuatayo.** **(alama 2)**

Vile vyote alivyovileta vitapikwa vile.

T/W T/E 2x1 = 2

q) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia – o – rejeshi ya mazoea. (alama 2)

Wale ambao wanafuzu vizuri hutia bidii masomoni.

Wale wafuzuo vizuri hutia bidii masomoni 2/0

r) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)

Mwalimu mgeni anafunza darasa lake.

Mwalimu (mgeni) hatakuwa amefunza darasa lake. 2/0

Mwalimu atakuwa hatafunza darasa lake

s) Tunga sentensi yenye kishazi tegemezi kinachochukua nafasi ya chagizo cha mahali. (alama 2)

Nguruwe amechafua anamolala. (po) 2/0

t) **Weka neno nywele katika ngeli mwafaka.** **(alama 1)**

U – ZI 1/0

u) **Andika methali anayoambiwa mtu anayefikiria kuwa ana vitu vingi na kuanza kuvitupatupa ovyo / kuvitumiatumia ovyo.** **(alama 1)**

Chovya chovya humaliza buyu la asali 1/0

Bandu bandu huisha (humaliza) gogo

14



14 + 12 + 14 = 40

Sarufi = 1 ugumu alama

Hijai = 6 x ½ = 3

## 4. ISIMUJAMII (Alama 10)

a) *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.*

"Mwanangu maji yangekuwa yamewafika shingo basi mngeshindwa kuishi pamoja. Ndoa ni bembea. Kuna wakati itakuwa juu na wakati itakuwa chini. Hizo juu-chini chini-juu ndizo utamu wake. Ni kama maisha kwa jumla. Yana pandashuka ndiyo lakini pandashuka hizo ndizo hutupa kuridhika hatimaye tunapozishinda. Hali hii itabadilika. Jikaze *dear*.

i. Hii ni sajili gani? Ushauri nasaha, mashauri (alama 1)

Mawaidha/ wosia/ nasaha/ nasiha/ ushauri 1/0

ii. Eleza sifa **nne** za sajili hii jinsi zinavyobainika kifunguni. (alama 4)

Kulinasibisha na mhusika – mwanangu.

Lugha ya matumaini – hali hii itabadilika. 4x1 = 4

Lugha mseto – Jikaze dear. / Kuchanganya ndimi.

Takriri / uradidi – juu-chini – chini-juu ili kusisitiza.

Lugha elezi – ili kufafanua vizuri.

Lugha sanifu – ili kuonyesha umuhimu wa ushauri. Mfano

Lugha shawishi ...basi mngeshindwa kuishi pamoja.

- Sentensi ndefu ndefu
- Kauli fupi fupi
- Lugha ya nyenyekevu / upole
- Tashbihi – lugha ya hisia, istiara
- Jazanda

b) Wewe ni mfanyabiashara rejareja. Eleza sifa za lugha utakayoitumia katika kutekeleza kazi yako. Sajili isiyo rasmi (alama 5)

Msamiati maalum – bei, wateja, bidhaa.

Lugha mseto – Nikuuzie ni mummy, welcome.

Utohozi – tochi ni mia.

Lugha shawishi – hii ukanunua utajilamba vidole daima

Misimu – hii ni mbao bei ya chini kuliko mkate

Uradidi – sabuni ni mia mia tu, karibu karibu

Lugha ya upole / bembelezi – karibu karibu baba, nikusaidie

Lugha legevu – nikuuzieko mkate mgani?

takriri / uradidi 5x1 = 5



Sanifu 4x½ = 2
Hiyai 4x½ = 2